

Halmashauri ya shule ya Jitihada ilijitolea mhanga kuzungumzia suala la afya. Wanafunzi walishauriwa kutorundika ovyo mabiwi ya taka. Ili kuimarisha afya yao, walihimizwa kupiga mafunda ya maji kila siku. Walifahamishwa kuwa mtungo wa samaki una protini inayoweza kujenga mwili. Vilevile tonge la ugali huupa mwili nguvu ya kufanya kazi. Aidha, kichala cha matunda na kicha cha mboga vina asilimia kubwa ya vitamini. Walihimizwa kutunza misitu ya miti ili kuhifadhi mazingira.